**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA**
**SHULE YA SEKONDARI MAHINA – MWANZA**

**Simu**
Mkuu wa shule: 0767 765076
Makamu Mkuu wa shule: 0754 398862
Mtaaluma: 0746703113
Matron: 0759468200
**Email**
mahinasekondari@gmail.com

**S. L. P 991**
**MWANZA**

\

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO BWENI WASICHANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI MAHINA - MWANZA



Draft



Grey

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA**
**SHULE YA SEKONDARI MAHINA**

**S. L. P 991,**
**MWANZA.**
**TAREHE: ………..…...**

**Kumb Na. MHNSS/MZ/ADM/2025**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi**
**………………………………….**
**………………………………….**

**<u>YAH</u>: <u>MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MAHINA BWENI WASICHANA HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA MKOA WA MWANZA MWAKA</u>** **<u>,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,</u>**

1. Nafurahi kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii kwa mwaka .......... na atasoma tahasusi ya …………………..

   Shule ya sekondari Mahina ipo umbali wa kilometa 04 kaskazini mwa Jiji la Mwanza. Usafiri wa bajaji kutoka stand ya mabasi (Buzuruga) unapatikana nauli ni shilingi 700/= na shilingi 2,000/= kwa pikipiki. Muhula wa masomo unaanza tarehe ………………………. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ……………………. Mwisho wa kuripoti ni tarehe ………………….

**2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia**

**2.1 SARE YA SHULE**

1. Shati mbili za tetroni nyeupe zenye mikono mirefu ambazo hazibani mwili na ziwe na mfuko mmoja kushoto. Zinavaliwa kwa kuchomekea
2. Sketi mbili ndefu inchi **sita (06)** kutoka magotini. Rangi ya sketi ni **Draft** kitambaa cha suti. Mshono ni boksi marinda moja kubwa katikati mbele na nyuma na rinda za kawaida tatu kushoto na tatu kulia. (kitambaa na mshono vimeambatanishwa)
3. Nguo za kushindia (shamba dress) jozi mbili mbili rangi ya **Grey (Kijivu)** kitambaa cha **sukarisukari.** Mshono ni linda Boksi kama ilivyo kwa sketi. (mshono na kitambaa vimeambatanishwa)
4. Sketi ndefu za rinda boksi inayovuka goti kwa **inchi sita (06)** kitambaa cha suti rangi ya **draft**, nusu kanzu ya kuvuka goti kitambaa cha tetroni na juba (Hijab) nyeupe (kwa wanafunzi wa kiislamu tu)
5. Sare za michezo ni **raba nyeupe** na track suit moja na jaketi lake rangi ya **Dark Blue**
6. Viatu vya shule ni vyeusi vya Ngozi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
7. Soksi jozi mbili zinazofika chini ya goti (**stocking**) na zisizo na pambo lolote.
8. Tai moja ya rangi nyeusi yenye michirizi myeupe.

9. Sweta moja rangi ya **dark blue** iwe na michirizi myeupe miwili mikononi na shingoni.
10. T – shirt moja ya rangi ya light blue yenye nembo ya shule.

**MUHIMU:** Ukipata Changamoto ya sare na vitambaa njoo shuleni vinapatikana.

**2.2 MAHITAJI MUHIMU**

i. Madaftari (8 kwa masomo ya Sanaa na 11 kwa masomo ya sayansi 3 Quire)
ii. **Ream A4 Double A (mbili)** na **Rulled paper 2** kwa mwaka
iii. **Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (orodha imeambatanishwa)**
iv. Dissecting kit 1 na koti jeupe la maabara kwa wanafunzi wanaosoma biology
v. **Scientific calculator kwa wanafunzi wa sayansi (fx 991 original); physics, chemistry, mathematics na geography.**
vi. Godoro futi 2½ (Deluxe / Comfy) lililotumika halitapokelewa
vii. **Mashuka pair 2 rangi ya pink, blanket 1, foronya ya godoro 1, Chandarua 1 (blue/nyeupe)**
viii. Nguo za ndani za kutosha
ix. **Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe)**
x. **Ndoo ndogo mbili zenye mfuniko**
xi. **Faili la plastiki 1**
xii. **Picha tatu (03) za passport zize**
xiii. **Nakala ya result slip ya Form IV na cheti cha kuzaliwa**
xiv. **Mahitaji mengine kwa tahasusi husika**
   **a) PCM (Mopa 1 na kindoo chake, na soft broom)**
   **b) HGL (Mopa na kindoo chake na chelewa 2)**
   **c) HKL (Brush za kusafishia choo 2 na jembe 1)**
   **d) CBG (Kwanja 1 na chelewa 2, mopa na kindoo chake)**

**Nb: Mahitaji haya unaweza kuyapata kwenye DUKA la shule ili kuepuka usumbufu wa mizigo mingi**

**2.3 MICHANGO MBALIMBALI**

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| **1** | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| **2** | Tahadhari | 5,000/= |
| **3** | Nembo | 5,000/= |
| **4** | Kitambulisho cha shule | 5,000/= |
| | **JUMLA** | **80,000/=** |

**Malipo yote yalipwe kupitia account hii 31101200131 NMB Kenyatta Branch. Jina la Account ni MAHINA SECONDARY SCHOOL**

## 3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE YA SEKONDARI MAHINA

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na:

### 3.1 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

i. Heshima kwa viongozi, wazazi na wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (preparation studies)
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wake katika shule hii
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule,
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
ix. Kutunza mali za shule
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.
xii. Kutofanya mitihani ya ndani na nje kwa makusudi

**MUHIMU**

❖ Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi
❖ Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kinatumiwa na mwanafunzi mmoja tu;
❖ Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa Ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa)

**3.2 MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku tisini (90) bila Taarifa/utoro
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule
vi. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
vii. Uvutaji wa sigara
viii. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kutolewa
ix. Kupata ujauzito au kutoa mimba
x. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi
xi. Kwenda kweye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni
xii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
xiii. Kudharau Bendera ya Taifa
xiv. Kufanya jambo lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu, na
xv. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4.0 VIAMBATANISHO NA FOMU MUHIMU**

i. Fomu ya uchunguzi wa afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali,
ii. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai,
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule, na
iv. Picha nne (4) za wazazi na Ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

**5.0 Tafadhali soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule:**

**Jina la Mkuu wa Shule:** **IBRAHIM OMAR KITIGWA**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule:** MKUU WA SHULE
MAHINA SEKONDARI
S. L. P. 991
NYAMAGANA_MWANZA

**OFISI YA WAZIRI TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA**

**SHULE YA SEKONDARI MAHINA**

## HISTORIA YA MWANAFUNZI

1. Jina la Mwanafunzi: ……………………………………………………………………
2. Shule ya Msingi uliyosomea ……………………………………………………………
3. Dini/Dhehebu ……………………………………………………………………………
4. Tarehe ya kuzaliwa ……………………………………………………………………
5. Anuani ya Mzazi/Mlezi …………………………………………………………………
6. Jina la baba ……………………………………………………………………………
7. Jina la mama ……………………………………………………………………………
8. Jina la Mtaa/Kijiji ……………………………………………………………………
9. Namba ya nyumba ………………………………………………………………………
10. Kazi aifanyayo baba …………………………………………………………………
11. Kazi aifanyayo mama …………………………………………………………………
12. Namba ya simu ya Mzazi/Mlezi ……………………………………………………
13. Kama huishi na Mzazi/Mlezi …………………………………………………………
14. Jina la Mlezi ……………………………………………………………………………
15. Jina la Mtaa/Jiji …………………………………………………………………………
16. Namba zingine za familia ……………………………………………………………

| Na | JINA LA MZAZI/MLEZI | UMRI | KAZI ANAYOFANYA | MAHALI ANAPOFANYIA KAZI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| 3 | | | | |
| 4 | | | | |

PASSPORT YA BABA

PASSPORT YA MAMA

PASSPORT YA MLEZI 1

PASSPORT YA MLEZI 2

**MWANAFUNZI**

Mimi ………………………………………………………………… ambae ni mwanafunzi niliyechaguliwa kujiunga na kidato cha tano tahasusi ya ……………….. katika shule hii ya Sekondari Mahina, naahidi Kufuata sheria, taratibu pamoja na miongozo iliyotolewa na itakayotolewa na uongozi wa shule.

Sahihi ya mwanafunzi ………………………………………………………… Tarehe ………………...

**MZAZI/MLEZI**

Mimi …………………………………………………………………… Ambae ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi …………………………………………………………………………….. nimeyasoma masharti na sheria za shule ya sekondari Mahina. Naahidi kwamba kipindi chote ambacho mwanangu atakapokuwa katika shule hii, nitamuhimiza na kumshauri kuzifuata sheria na taratibu za shule kama zilivyotolewa na zitakavyotolewa na uongozi wa shule. Aidha, naahidi kushirikiana na uongozi wa shule katika mambo mbalimbali ya kitaaluma yanayomhusu mwanangu na kumpatia malezi bora.

Sahihi ya Mzazi/Mlezi ………………………………………………………… Tarehe ………………...

**IJAZWE NA MWENYEKITI/MTENDAJI WA SERIKALI ZA MITAA**

JINA KAMILI LA MWENYEKITI: ………………………………………………………………………..

CHEO: ………………………………………...……………………………………………………..

NAMBA YA SIMU: ……………………………...…………………………………………………….

SAHIHI: ……………………… MHURI:

# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

## PRIME MINISTER'S OFFICE - RALG

## MEDICAL EXAMINATION FORM

MAHINA SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 991
MWANZA
......../…../……….

TO THE MEDICAL OFFICER
...............................................................
...............................................................
................................................................

NAME OF THE STUDENT: ……………………………………………………………………………

Please examine the name mentioned and recommend if she / he is fit / unfit to pursue secondary education.
Stool.........................................................................................................................................
Blood BP.....................................................................................................................................
Urine.........................................................................................................................................
Chest TB.....................................................................................................................................
Eye sight.....................................................................................................................................
Pregnancy Test...........................................................................................................................

Any other physical disability not listed that may affect his/her studies
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………..

Medical information e.g Physical defect / impairment(s) chronic disease requiring special attention / care.
I certify that I have examined the above student and recommend that he / she is fit / unfit to pursue secondary education.

Signed...........................................

Designation.................................... Official Stamp..............................

Date..............................................